## ACT YAMPONGEZA TUNDU LISSU

## WAKAZI ZAIDI YA 1,000 MPIJI MAGOE KUNUFAIKA NA MAJISAFI

kumekucha @kumekucha @kumekucha





# KUMEKUCHA

Tovuti www.kumekucha.co.tz/ ISSN 4562-9710. NA. 08, Alhamisi Januari 23, 2025 Bei Tsh. 1,000/= Ksh 100


# DK. MWINYI ATIKISA ZANZIBAR

Dkt Mwinyi alisema ushindi mwingine uliompa fursa ya kugombea Urais wa Zanzibar umewaacha midomo wazi wafitini, waliokuwa wakidai kwamba hatoweza...uk.2

>> MAELFU WAMLAKI KWA KISHINDO

>> ASEMA HANA HOFU NA WAPINZANI



## MBOWE AACHA WOSIA MZITO CHADEMA




## JOHN MNYIKA ABAKIZWA UKATIBU MKUU CHADEMA

## BENKI KUU YANUNUA TANI 2.6 ZA DHAHABU

# DK.MWINYI AIBUA SHANGWE ZANZIBAR

NA MWANDISHI WETU, ZANZIBAR

ILIKUWA ni shamra shamra na nderemo kila kona kisiwabi Zanzibar baada ya kuwasili mgombea wa kiti cha Urais wa Chama Cha Mapinduzi Zanzibar, ambaye pia ni Rais wa sasa Dkt Hussein Mwinyi akitokea Makao Makuu ya chama hicho Mjini Dodoma.

Mwinyi amechaguliwa kuendelea kugombea nafasi ya Urais kupitia tiketi ya CCM katika Mkutano MKuu Maalum wa CCM uliofanyika Ukumbi wa Jakaya Kikwete Jijini Dodoma, na jana ilikuwa ndiyo siku yake ya kurejea Zanzibar, ambapo maelfu ya wakazi wa Zanzibar walijipanga katika barabara mbalimbali ulipopita msafara wake na kisha kuzungumza na wananchi akitoa shukurani zake kwa mapokezi hayo.

Dkt Mwinyi alisema,ushindi mwingine uliompa fursa ya kugombea Urais wa Zanzibar umewaacha midomo wazi wafitini, waliokuwa wakidai kwamba hatoweza kurejea tena kugombea nafasi hiyo kutokana na kutokubalika.

Mamia ya Wananchi wa Zanzibar na Wana CCM walijitokeza kwa Wingi Pembezoni mwa Barabara kuu ya Uwanja wa Ndege- Kilimani kumpokea Dk ,Mwinyi aliyekuwa katika Gari la Wazi akiwapungia Mkono hadi Afisi Kuu ya CCM Kisiwandui.

Mgombea Mteule wa Urais wa Zanzibar Dk.Hussein Ali Mwinyi alizuru Kaburi la aliyekuwa Rais wa Kwanza wa Zanzibar Hayati Abeid Amani Karume na Kuweka Shada la Maua pamoja na Kuzungumza na Wazee wa Chama cha Mapinduzi na Kumpongeza pamoja na kumtakia Kila la Heri katika safari yake ya Kinyang'anyiro cha Urais wa Zanzibar.

Akizungumza na Wana CCM na Wananchi Uwanja wa Mapinduzi Square, Michenzani Dk. Mwinyi ameeleza kuwa CCM imemaliza kazi ndani ya Chama ya Kufanya Maamuzi sahihi ya kupata Wagombea wake na kazi iliobaki ni ya kutafuta ushindi wa kishindo Mwezi wa Oktoba katika Uchaguzi Mkuu.

Dk.Mwinyi amekishukuru Chama Cha Mapinduzi Kupitia ngazi zote kwa kuthamini Kazi ya Utekelezaji wa Ilani iliyofanywa naye pamoja na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan na kuwateua tena kuwa Wagombea wa Chama hicho.

Makamu Mwenyekiti wa CCM Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi amewasisitiza Wana CCM na Wananchi kujiandikisha katika Daftari la Wapiga Kura litakapoanza Mwezi Februari Mwaka huu na hatimaye kujitokeza kupiga Kura Mwezi Oktoba ili Chama Cha Mapinduzi kipate ushindi wa kishindo.

Aidha amewasisitiza kuendelea Kutunza Amani na Utulivu wa Nchi Hususani Wakati huu wa Kuelekea Uchaguzi Mkuu.

## NOTI MPYA KUANZA KUTUMIKA FEBRUARI MOSI

Na Benny Mwaipaja,

GAVANA wa Benki Kuu ya Tanzania,Emanuel Tutuba amesema kuwa Noti Mpya za Tanzania zenye Saini ya Waziri wa Fedha,Dk. Mwigulu Lameck Nchemba na yeye mwenyewe, za toleo la mwaka 2010, zitaingia kwenye mzunguko kuanzia tarehe mosi Februari mwaka huu.

Gavana Tutuba amesema hayo wakati akimkabidhi,Dk.Nchemba, Noti kifani za shilingi elfu kumi, elfu Tano, Elfu Mbili na Shilingi Elfu moja, katika Ofisi Ndogo za Wizara ya Fedha, Jijini Dar es Salaam, kwa mujibu wa Sheria na Taratibu zinazosimamia masuala ya fedha nchini.

“Mheshimiwa Waziri, ninayofuraha kukujulisha kuwa zoezi letu la uchapaji upya wa Noti kwa marejeo ya toleo la mwaka 2010, limekamilika na tayari tumewajulisha wananchi kupitia taarifa niliyoitoa kupitia Gazeti la Serikali” alisema Bw. Tutuba.

Gavana Tutuba alifafanua kuwa Noti hizo zitatumika sambamba na Noti zilizopo hivi sasa, zinamwonekano wa Noti zinazotumika hivi sasa zilizotolewa Mwaka 2010, ikiwemo alama za usalama, ukubwa, rangi na mambo mengine, isipokuwa ina marekebisho kwenye saini ya Waziri wa Fedha, na Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania.

“Saini ya aliyekuwa Waziri wa Fedha ambaye hivi sasa ni Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,Dk.Philip Isdor Mpango imebadilishwa na kuwekwa Saini yako Dk.Mwigulu Lameck Nchemba na Saini ya aliyekuwa Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania aliyestaafu,Prof. Florens Luoga, imebadilishwa na kuwekwa Saini ya Gavana wa Benki Kuu wa sasa, Bw. Emmanuel Tutuba” aliongeza Bw. Tutuba.

Akizungumza baada ya kupokea sampuli za Noti hizo mpya, Waziri wa Fedha,Dk.Mwigulu Lameck Nchemba,alimshukuru,Rais Dk.Samia Suluhu Hassan kwa kuruhusu jambo hilo kufanyika na kumpongeza Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Emmanuel Tutuba, kwa kusimamia mchakato wa uchapaji wa Noti hizo kwa weledi na uadilifu mkubwa.

“Mpaka kufikia hatua hii ni heshima kubwa kwa Taifa letu na inaendeleza heshima ya wataalam wetu mnavyoweza kusimamia kwa umakini mambo yenye maslahi mapana kwa nchi yetu” Alisema Dk. Nchemba.

Dk.Nchemba aliridhia Noti hizo ziingizwe kwenye mzunguko na kuanza kutumika kama ilivyopangwa tarehe moja Februari mwaka huu.

## JOHN MNYIKA ABAKIZWA UKATIBU MKUU CHADEMA

NA HUSNA NASSORO

MWENYEKITI Mpya wa CHADEMA,Tundu Lissu akiwa kwenye Mkutano wa Baraza Kuu la Chama ambalo limekutana jana jijini Dar es Salaam,katika ukumbi wa Mlimani City,ameanza kupanga safu ya uongozi kwa kumteua John Mnyika kuendelea na cheo Katibu Mkuu.

Kwa mujibu wa Taarifa iliyotolewa na Chama hicho,Mnyika ataendelea na wadhifa huo hukua akisaidiwa na Manaibu Makatibu Wakuu wawili.

Aman Golugwa ndiye anayekwenda kuwa Naibu Katibu Mkuu Tanganyika (Tanzania Bara)na Wakili Ally Ibrahim Juma,Naibu Katibu Mkuu Zanzibar.

Aidha Lissu amewateua Godbless Lema,Dk. Rugemeleza Nshala,Mwanasheria Mkuu wa Chama,Rose Mayemba,Salma Musa Kasanzu na Hafidh Ally Salehe kuwa wajumbe wa Kamati Kuu.

## ACT YAMPONGEZA TUNDU LISSU

NA HUSNA NASSORO



CHAMA cha ACT Wazalendo kimeonyesha ukomavu wa kisiasa kwa kumpongeza Tundu Lissu kufuatia ushindi wake kama Mwenyekiti wa CHADEMA, nafasi ambayo pia inamfanya kuwa Mwenyekiti wa Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD).

Kupitia ujumbe uliochapishwa na ACT Wazalendo kwenye ukurasa wao wa X (zamani Twitter), kiongozi wa chama hicho, Mwl. Macheyeki Philbert Jr, amepongeza Lissu kwa ushindi huo na kumkaribisha katika uongozi wa TCD, akiahidi ushirikiano wa dhati katika harakati za kuimarisha demokrasia nchini.

Lissu alishinda uchaguzi Mkuu wa CHADEMA juzi kwa kumgaragaza aliyekua Mwenyekiti wake Freeman Mbowe huku John Heche akishinda nafasi ya Makamu Mwenyekiti.



# MBOWE AACHA WOSIA MZITO CHADEMA

NA ILHAM JUMA



MWENYEKITI mstaafu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Freeman Mbowe amesema uchaguzi wa viongozi ndani ya chama hicho umeacha majeraha mengi miongoni mwa wanachama.

Kufuatia hali hiyo, Mbowe ameshauri viongozi walioingia madarakani kukiponya chama hicho kutokana na majeraha hayo.

Amesema yeye aliahidi angeshinda nafasi ya Uenyekiti angeunda Tume ya Ukweli na Upatanishi ili watu wakazungumze yaliyojiri kuelekea uchaguzi huo ambapo pale watu walipokoseana adabu, walipokosa nidhamu, walipokosa maadili, walipokibagaza chama hicho wakasameheane, wapeane mikono ili CHADEMA ikawe yenye nguvu zaidi.

Mbowe ameyasema jana katika Ukumbi wa Mikutano wa Mlimani City, Dar es Salaam baada ya kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi wa viongozi wa kitaifa wa chama hicho.

"Ni kweli tumefanya uchaguzi jana hadi leo uliokuwa huru, wa wazi, wa haki ambayo kila binadamu mwenye akili timamu ameiona. Uchaguzi kuwa huru, wa haki, na wa wazi halipaswi kuwa tukio la siku moja, linapaswa kuwa mchakato wote unaojenga hadi siku ya kesho",

"Nimesema mara nyingi na ninasema tena, kwa namna ambavyo wagombea mbalimbali na mashabiki wao walivyojinasibu katika kujenga kampeni za uchaguzi huu, kampeni zimeziachia chama chetu majeraha makubwa, na hili ni jambo ambalo WanaCHADEMA tusipolikubali na kulitibu, tutaumiza 'brand' ya chama chetu ambayo tunapaswa wote kuilinda... lakini ambacho ni kweli na tunapaswa tukiseme ni kwamba uchaguzi huu umeacha majeraha mengi ndani mwetu". amesema Mbowe.

## WAKAZI ZAIDI YA 1,000 MPIJI MAGOE KUNUFAIKA NA MAJISAFI

NA MWANDISHI WETU

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es salaam (DAWASA) inaendelea na utekelezaji wa mradi wa maji Mpiji Magoe katika kata ya Mbezi Wilayani Ubungo wenye lengo la kutatua adha ya maji na kuhudumia kaya takribani 1,000

Akizungumza utekelezaji wa mradi huo, Mhandisi msimamizi wa mradi, Agness Kenani amesema mradi wa maji Mpiji Magoe unaotekelezwa kwa gharama ya Shilingi Milioni 877 unakwenda kujibu changamoto ya maji katika eneo hilo lililokuwa halina mtandao wa Maji DAWASA.

“ Utekelezaji wa mradi huu umeanza mwezi Agusti, 2024 na unajumuisha uchimbaji na ulazaji wa bomba za ukubwa wa inchi 8 na inchi 6 kwa umbali wa Kilomita 7, kazi hii mpaka sasa ipo zaidi ya asilimia 25 na kazi zinaendelea kwa kasi” alifafanua

Mhandisi Agness amesema baada ya mradi kukamilika Wananchi wa eneo hilo watasahau matumizi ya maji chumvi yatokanayo na visima na watakua na uhakika wa Majisafi na salama.

Kwa upande wake, Mjumbe wa serikali ya mtaa wa Mpiji Magoe, Honest Peter amewashukuru DAWASA kwakuwa wasikivu na kuja na suluhisho la huduma ya maji kupitia mradi huu.

"Tulipofikisha mahitaji yetu DAWASA, wamekuwa wasikivu na kutoa ushirikiano, leo tunaona mradi unatekelezwa kwa kasi na tumeshapokea sehemu ya mabomba kwajili ya mradi huu," amesema Honest

Honest amesema eneo la Mpiji walisumbuka na huduma ya maji kwakua eneo kubwa halikua na mtandao wa DAWASA, lakini sasa wananchi wana matumaini makubwa ya kupata huduma bora ya majisafi.

Esther Daudi, mkazi wa mtaa wa Mpiji Magoe amepongeza jitihada zinazofanyika kuwapatia huduma ya majisafi wananchi wa eneo hilo na kuomba mradi utekelezwe kwa kasi zaidi ili uweze kuleta tija kwa wakazi wa eneo hilo na kufurahia huduma ya majisafi.

Mradi wa maji Mpiji Magoe utanufaisha wakazi wa maeneo ya Machimbo, Mpiji Centre, Mpiji CCM, Masaki Ndogo, Bedisaida, Kwa Mzungu pamoja na Torino huku ukienda kuhudumia wateja zaidi ya 1,000 kwa kuwapatia huduma bora ya majisafi na salama.

# BENKI KUU YANUNUA TANI 2.6 ZA DHAHABU

NA MWANDISHI WETU

WAZIRI wa Madini,Anthony Mavunde,amebainisha kuwa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imenunua tani 2.6 za dhahabu inayochimbwa na kusafishwa hapa nchini ikiwa ni sehemu ya juhudi za kukabiliana na changamoto ya upungufu wa fedha za kigeni, kuboresha akiba ya fedha za kigeni, na kuimarisha thamani ya shilingi ya Tanzania.

Mavunde ameyasema hayo,jijini Dodoma, wakati akiwasilisha taarifa kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, taarifa inayohusu utendaji wa viwanda vya kusafisha dhahabu nchini kwa kipindi cha Machi hadi Desemba 2024 pamoja na mwenendo wa ununuzi wa dhahabu unaotekelezwa na BoT.

Kwa mujibu wa Waziri Mavunde,Oktoba Mosi 2024, Tume ya Madini ilitoa tangazo linalowataka wachimbaji na wafanyabiashara wa dhahabu kutekeleza takwa la Kifungu cha 59 cha Sheria ya Madini Sura 123, ambalo linawataka kutenga asilimia 20 ya dhahabu na kuiuzia BoT kupitia viwanda vya usafishaji vilivyoidhinishwa.

“Mheshimiwa Mwenyekiti, Tangu kutolewa kwa tangazo hilo hadi Januari 21, 2025, BoT imefanikiwa kununua tani 2.6 za dhahabu kutoka kwa wachimbaji wa kati, wachimbaji wadogo, na wafanyabiashara wa dhahabu.

Thamani ya dhahabu hiyo ni zaidi ya shilingi bilioni 570 kwa mujibu wa bei ya soko la dunia ya tarehe 22 Januari 2025” amesema,Mavunde.

Halikadhalika, Waziri Mavunde amesisitiza kuwa, kupitia mpango huo wa BoT, lengo la Serikali ni kuifanya Tanzania kuwa moja ya mataifa 10 yenye hifadhi kubwa ya dhahabu barani Afrika kwa ustawi wa taifa.

Ongezeko la Mapato ya Serikali

Kwa upande wa mapato, Waziri Mavunde amebainisha kuwa, mwenendo wa ukusanyaji wa mrabaha kwa upande wa madini ya dhahabu umeendelea kuimarika na kwamba kuanzia Julai 1, 2024 hadi Desemba 31, 2024, Serikali iliingiza shilingi bilioni 400.22 kutokana na mauzo ya kilogramu 34,826.75 za dhahabu, ikiwa ni ongezeko la asilimia 5.55 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2023, ambapo kilogramu 32,995.54 ziliuzwa na Serikali kupata shilingi bilioni 278.86.

# MBOWE AACHA WOSIA MZITO CHADEMA

NA ILHAM JUMA



MWENYEKITI mstaafu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Freeman Mbowe amesema uchaguzi wa viongozi ndani ya chama hicho umeacha majeraha mengi miongoni mwa wanachama.

Kufuatia hali hiyo, Mbowe ameshauri viongozi walioingia madarakani kukiponya chama hicho kutokana na majeraha hayo.

Amesema yeye aliahidi angeshinda nafasi ya Uenyekiti angeunda Tume ya Ukweli na Upatanishi ili watu wakazungumze yaliyojiri kuelekea uchaguzi huo ambapo pale watu walipokoseana adabu, walipokosa nidhamu, walipokosa maadili, walipokibagaza chama hicho wakasameheane, wapeane mikono ili CHADEMA ikawe yenye nguvu zaidi.Mbowe ameyasema jana katika Ukumbi wa Mikutano wa Mlimani City, Dar es Salaam baada ya kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi wa viongozi wa kitaifa wa chama hicho.

"Ni kweli tumefanya uchaguzi jana hadi leo uliokuwa huru, wa wazi, wa haki ambayo kila binadamu mwenye akili timamu ameiona. Uchaguzi kuwa huru, wa haki, na wa wazi halipaswi kuwa tukio la siku moja, linapaswa kuwa mchakato wote unaojenga hadi siku ya kesho",

"Nimesema mara nyingi na ninasema tena, kwa namna ambavyo wagombea mbalimbali na mashabiki wao walivyojinasibu katika kujenga kampeni za uchaguzi huu, kampeni zimeziachia chama chetu majeraha makubwa, na hili ni jambo ambalo WanaCHADEMA tusipolikubali na kulitibu, tutaumiza 'brand' ya chama chetu ambayo tunapaswa wote kuilinda... lakini ambacho ni kweli na tunapaswa tukiseme ni kwamba uchaguzi huu umeacha majeraha mengi ndani mwetu". amesema Mbowe

# KAMATI YA BUNGE YAIPA 5 OFISI YA WAZIRI MKUU

NA MWANDISHI WETU

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii imeridhishwa na utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zake kwa namna inavyowagusa wananchi, huku ikimpongeza Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa juhudi zake za kukuza ustawi na maendeleo ya Watanzania.

Pongezi hizo zimetolewa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Fatuma Toufiq, jijini Dodoma wakati ikipokea taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kwa kipindi cha Julai hadi Desemba 2024.

Kwa upande wake, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Ridhiwani Kikwete, amesema ofisi hiyo katika mwaka wa fedha 2024/2025 imepanga kuendelea kutekeleza shughuli mbalimbali, zikiwemo usimamizi wa kazi na huduma za ukaguzi, maendeleo ya vijana, kuratibu shughuli za ajira, utoaji wa huduma kwa watu wenye ulemavu, hifadhi ya jamii, na ukuzaji wa tija.

Ameahidi kuwa ofisi hiyo itatekeleza majukumu hayo kikamilifu ili kufanikisha malengo yaliyowekwa.

## TANAPA YAZINDUA VALENTINE WEEKEND GATEWAY

Na Philipo Hassan - Mwanza

SHIRIKA la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) kwa kushirikiana na Kampuni ya Busybee imezindua Kampeni yake ijulikanayo Valentine Weekend Gateway jijini Mwanza, lengo likiwa ni kuhamasisha Watanzania na wasio Watanzania kutembelea Hifadhi za Taifa kipindi hiki cha msimu wa Sikukuu ya Wapendanao.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa uzinduzi, Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi Jully Lyimo, anayeshughulikia Kitengo cha Maendeleo ya Biashara TANAPA Makao Makuu, alianza kwa kufunga rasmi kampeni ya Shangwe la Sikukuu na TANAPA iliyozinduliwa Disemba 01, 2024 Jijini Arusha.

Kamishna Lyimo alieleza mafanikio ya kampeni hiyo kwa kutaja ongezeko kubwa la watalii wa ndani: “Kampeni ya Shangwe la Sikukuu na TANAPA ilifanikiwa kuvuka lengo la awali ambalo lilikuwa ni kupata watalii wa Kitanzania na 28,000.”

Kamishna Lyimo Aliongeza: “Jumla ya Watanzania 36,933 walitembelea Hifadhi za Taifa kuanzia tarehe (1/12/2024 hadi 5/1/2025), sawa na ongezeko la asilimia 44% ukilinganisha na Watalii waliotembelea katika kipindi kama hicho kwa mwaka jana (1/12/2023 hadi 5/1/2024).”

Akizungumzia dhima ya uzinduzi wa kampeni mpya ya Valentine Weekend Gateaway na TANAPA, Kamishna Lyimo alisema, “Leo tunazindua kampeni hii kwa Hifadhi zote 21, tunawahamasisha Watanzania wote watembelee Hifadhi zetu maana tumeandaa vifurushi rafiki vya bei nafuu vinavyomwezesha kila Mtanzania kumudu gharama za kutalii msimu wa wapendanao.”

Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi,Dk. Tutindaga Mwakijambile,Mkuu wa Hifadhi ya Taifa Kisiwa cha Saanane, alitoa maelezo kuhusu Kisiwa cha Saanane ambapo ni mahali pa kipekee kwa wapendanao. Mandhari tulivu, fursa za kipekee za kupumzika, na shughuli mbalimbali za kuburudisha zinazotengeneza uzoefu wa kukumbukwa milele.

Kamishna Dk.Tutindaga aliongeza, “tumejiandaa kuwahudumia wapendanao, Watalii wataweza kutembelea Kisiwa cha Saanane chenye msitu wa kijani uliosheheni miamba minene ya mawe iliyobanana, wanyama kama Swala, Nyumbu, Simba, Mamba, na Ndege wa aina mbalimbali pamoja na mandhari nzuri ya jiji la Mwanza.”

Mkurugenzi wa Kampuni ya Busybee, Baraka Nyororo, alieleza kwa upana kuhusu ushirikiano na TANAPA katika kuandaa tukio hilo adhimu katika jiji la Mwanza, ambapo Watanzania wengi wanatarajiwa kushiriki kutembelea kisiwa hicho siku ya Februari 15, 2025

Baraka alisema, “Tutaandaa tukio la Usiku mzuri kwa wapendanao ambapo watafurahia Night Excursion, Valentine Romantic Dinner, Bonfire, Games, burudani ya Muziki, matembezi ya miguu pamoja na kutazama nyota wakati wa usiku.”



# HOJA SABA ZILIZOMBEBA LISSU KUMNG'OA MBOWE



MWENYIKITI MPYA WA CHADEMA TUNDU LISSU

NA HUSNA NASSORO

TUNDU Lissu ndiye Mwenyekiti mpya wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).Amechukua nafasi ya mtangulizi wake Freeman Mbowe ambaye aliangukia pua katika uchaguzi Mkuu wa chama hicho uliofanyika Jumanne wiki hii Ukumbi wa Mlimani City,jijini Dar es Salaam.

Itakumbukwa kabla ya uchaguzi huo kulikuwa na mnyukano mkali wa hoja baina ya Mbowe na Lissu lakini pia wawili hao walirushiana makombora ya kashfa ambayo yaliwafanya wachambuzi wa masuala ya siasa kuona chama hicho kinajichimbia kaburi.

Ni kama wengi hawakutarajia Lissu angemshinda Mbowe lakini ukweli kila mgombea katika nafasi hiyo ya Uenyekiti alikua na hoja zake kwa ajili ya kuwashawishi wajumbe wa Mkutano Mkuu wampigie kura.Hizi hapa ni hoja saba zilizombeba Lissu mbele ya wajumbe wa Mkutano Mkuu wamuamini kumpigia kura akalie kiti cha nafasi ya Uenyekiti.

Sera za Tundu Lissu ndani ya CHADEMA zimekuwa zikijikita katika misingi ya demokrasia, uwajibikaji, utawala bora, na haki za binadamu. Hapa chini ni baadhi ya mambo makuu ambayo yameonekana kama sehemu ya msimamo na maono yake kwa chama na taifa:

**1. Kuimarisha Demokrasia ya Ndani ya Chama**

Lissu amekuwa akisisitiza uwazi na ushirikishwaji wa wanachama wote katika maamuzi ya chama.

Amehimiza kuhakikisha kuwa uchaguzi wa ndani wa CHADEMA unakuwa huru, wa haki, na unazingatia demokrasia.

Anapigania maoni ya wanachama wa kawaida kusikilizwa na kufanyiwa kazi.

**2. Kupigania Haki za Kikatiba**

Tundu Lissu amekuwa mstari wa mbele kutetea mabadiliko ya katiba ya Tanzania, akisisitiza umuhimu wa CHADEMA kuongoza juhudi za kuhamasisha wananchi kudai katiba mpya yenye msingi wa demokrasia ya kweli.Anaamini kuwa katiba mpya ni njia ya kuhakikisha utawala wa sheria na haki za raia.

**3. Kupambana na Rushwa na Udikteta**

Lissu amejikita katika kupinga rushwa ndani na nje ya chama, akitaka viongozi wa CHADEMA waonyeshe mfano wa maadili mema.

Ameweka wazi msimamo wake wa kupinga udikteta wa aina yoyote, ndani ya chama au kwenye ngazi ya taifa.

**4. Kuimarisha Ushirikiano wa Kimataifa**

Lissu ana mtazamo wa kuimarisha uhusiano wa CHADEMA na vyama vingine vya siasa na mashirika ya kimataifa yanayotetea demokrasia na haki za binadamu.Anaamini kuwa msaada wa kimataifa unaweza kusaidia chama kupata rasilimali na uzoefu wa kuimarisha kampeni za kisiasa na maendeleo ya chama.

**5.Uimarishaji wa Uchumi wa Chama na Wanachama**

Amezungumzia umuhimu wa kuimarisha uchumi wa chama ili kiweze kujiendesha bila utegemezi mkubwa kutoka kwa wafadhili.Anapendekeza kuwepo kwa mipango ya kusaidia wanachama kiuchumi kupitia ushirika na miradi mbalimbali ya kiuchumi.

6.Kuimarisha Ushirikiano na Wananchi

Lissu anaamini kuwa CHADEMA inapaswa kuwa karibu zaidi na wananchi kwa kusikiliza matatizo yao na kuyatafutia suluhisho.Amehimiza chama kuwekeza katika programu za kijamii ambazo zitawafanya wananchi waone thamani ya CHADEMA katika maisha yao ya kila siku.

**7. Kupambana kwa Ujasiri kwa Ajenda ya CHADEMA**

Ametoa wito wa chama kuendelea kupambana kwa nguvu zote kuhakikisha haki ya kushiriki siasa kwa uhuru inapatikana Tanzania.

Anaamini kuwa ujasiri wa kupigania ajenda za kidemokrasia ndio utakaowafanya wananchi waamini na kuunga mkono CHADEMA zaidi.

Kwa ujumla, sera zake zililenga kuimarisha chama, demokrasia, na ustawi wa wananchi wa Tanzania kwa ujumla.

# VYANZO VYA WIVU WA MAPENZI ULIOPINDUKIA

WIVU wa mapenzi uliopindukia husababishwa na vyanzo 6 kama ifuatavyo



### 1.MATATIZO YA KIAFYA

Changamoto za kiafya zenye kuchochea migogoro ya kimapenzi inayotokana na WIVU WA MAPENZI uliopindukia ni kama vile

#Kupoteza hisia za mapenzi mara kwa mara au kwa muda mrefu kutokana na kuugua muda mrefu sana bila kupata nafuu, kuugua mara kwa mara, kusumbuliwa na ugonjwa sugu kama shinikizo la damu, ugonjwa wa moyo, kisukari, uvimbe, saratani,

#Kusumbuliwa na ugonjwa sugu kama vidonda vya tumbo,kuumwa kichwa na mgongo, ulemavu wa kudumu, upungufu wa nguvu za kiume,ugumba, hedhi kuvurugika mara kwa mara, ujauzito kuharibika mara kwa mara,kutokwa na uchafu wenye harufu mbaya sehemu za siri,fungus sugu ukeni, ukavu sehemu za siri, fistula.

#kufanyiwa upasuaji (baadhi ya wanawake hujichukia wakiona alama za upasuaji tumboni) ,njia ya uzazi kuongezeka (baadhi ya wanawake hujichukia njia ikiwa pana)

#kusumbuliwa na ugonjwa usiokuwa na tiba kama ukimwi,

### 2.KUJICHUKIA KWA MUONEKANO PAMOJA NA UPWEKE WA MUDA MREFU

Unaweza kusumbuliwa na wivu wa mapenzi uliopindukia kwa sababu ya kujichukia kwa muonekano wako kwa vyanzo vifuatavyo

MWANAMKE

Mwanamke anaweza kujichukia kwa muonekano wake kwa sababu anajiona mfupi sana au mrefu sana,kujiona mnene kupita kiasi au mwembamba sana, kukosa umbo (shapeless),kujiona mzee kabla ya umri.

#kujiona yupo na sura ya kiume,sauti ya kiume,kujiona yupo na mpangilio usiovutia wa macho, pua, mdomo, meno, kucha, nywele, rangi ya ngozi,saizi ya maziwa n.k hivyo mara kwa mara anakuwa na hofu ya kuachwa mpweke,hofu ya kusalitiwa,hofu ya kukosa mwanaume mbadala kama akiachwa.

### MWANAUME ANAWEZA KUJICHUKIA KWA MUONEKANO KWA SABABU

Mwanaume kujiona mzee sana kabla ya umri,kujiona mwembamba sana au mnene kupita kiasi, ulemavu wa kudumu,kujiona mfupi sana au mrefu sana (hauendani na urefu wa Mwanamke wake)

Kujichukia kwa sababu ya muonekano usiovutia wa macho, pua, mdomo, meno, kucha, nywele,kichogo,

Uume mfupi sana (kibamia),kuota maziwa,sauti ya kike,uhalaza (bald head)

### UPWEKE NA MSONGO WA MAWAZO

Mwanaume au mwanamke anaweza kusumbuliwa na hofu ya kuachwa mpweke, pamoja na hofu ya kusalitiwa kwa sababu ya msongo wa mawazo pamoja na upweke wa muda mrefu hivyo anajiona mkosaji, kujiona kituko, kujiona kichekesho, kujiona mzigo,kujiona takataka,kujiona hana thamani kutokana na hali hiyo anakuwa anaibua ugomvi wa mara kwa mara au kulalamika ananyanyaswa kila siku.

### 3.MATATIZO YA KIFEDHA

Mwanaume au mwanamke anaweza kusumbuliwa na wivu wa mapenzi uliopindukia kwa sababu ya matatizo ya kifedha.Mara nyingi fedha humuathiri mwanaume lakini wapo wanawake huathiriwa na uhaba wa fedha katika mahusiano yao hasa wale wenye kuwalea wanaume (sugar Mommy/ mishangazi)

Uhaba wa fedha husababisha hofu ya kuachwa mpweke, pamoja na kusalitiwa kwa sababu unakuwa unahisi wenye uwezo mkubwa wa kifedha wanaweza kumchukua mwenza wako kwa urahisi.

### 4.MIGOGORO AMBAYO INAENDELEA HIVI SASA

Wivu wa mapenzi uliopindukia unaweza kusababishwa na migogoro ambayo inaendelea hivi sasa kama vile uonapo mwenza wako anaomba fedha nyingi sana kuliko uwezo wako,anatishia kukuacha ghafla kama hauna fedha,anatoroka kwenda kwao mara kwa mara,ameanza mawasiliano na mwenza wake wa zamani ( ex wake).

Lakini piaamekuwa na hasira kupita kiasi,ameanza kukufokea,kukutukana, kukudhalilisha hadharani, kukuita majina ya udhalilishaji, kukujibu vibaya,kupuuza simu zako,kukujibu kwa mkato,kudai muachane au mpeane nafasi hali hiyo husababisha unaanza kuhofia kuachwa mpweke au kusalitiwa. Vilevile kama mwenza wako anataka kusafiri siku za karibuni utaanza kuhofia kusalitiwa.

### 5.MAWASILIANO KUPUNGUA PAMOJA NA MAHUSIANO YA MBALI (LONG DISTANCE RELATIONSHIP)

Hofu ya kuachwa mpweke pamoja na kusalitiwa huongezeka pale ambapo unapiga simu mfululizo na kutuma sms mfululizo kwa mwenza wako lakini simu haipatikani au inaita lakini hapokei na sms hajibu lakini unaona yupo online anajibu sms za watu wengine pamoja na kubadilisha "WhatsApp status"

Vilevile hofu ya kuachwa mpweke pamoja na kusalitiwa huzidi kuongezeka kama kimepita kimya cha siku,wiki, wiki mbili mpaka mwezi hakuna mawasiliano yoyote na mwenza wako na hakuna ndugu zake yeyote anatoa ushirikiano wowote kwako. Hasa kama yupo chuoni au anafanya kazi nje ya wilaya, mkoa au nchi tofauti na makazi yako.



# NIMEUMIZWA NA USHINDI WA TUNDU LISSU

LUCAS MWASHAMBWA,



UCHAGUZI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo(CHADEMA) umemalizika na rasmi Tundu Lissu ndiye aliyechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa chama hicho huku John Heche akitwaa nafasi ya Makamu Mwenyekiti wake.

Ushindi huo umeniumiza,kunisikitisha ,kunihuzunisha na kunisononesha sana.Ni ushindi ambao unaiweka CHADEMA katika hatari ya kusambaratika,

ni ushindi ambao utapelekea kupoteza wanachama wengi kutokana na misuguano ya ndani kwa ndani. Ni ushindi ambao haukustahili kuelekea mikononi mwa watu kariba ya Lissu na Heche.

Hao watu wana ni waropokaji,wabaguzi sana na wenye mioyo iliyo jaa sumu ya chuki kubwa sana vifuani pao. Mimi binafsi namchukia sana Lissu siyo kwa sababu yupo CHADEMA nami nipo CCM.Namchukia Lissu kwa sababu ya Uropokaji wake.

Mdomo wa Lissu mara nyingi umetumika kuchochea sana na kupandikiza chuki ,uhasama na ubaguzi hapa Nchini.Ameutumia Mdomo wake bila Breki kumtukana na kumbagua Rais wetu. Kiasili mimi sipendi mtu mbaguzi na mwenye chuki kama aliyonayo lissu kifuani pake.

Sijawahi kufurahishwa wala kupenda namna Lissu alivyokuwa akimdhalilisha Rais wetu majukwaani kwa sababu ya Uzanzibari wake na uwanamke wake. Kwa sababu mimi naamini uongozi au kiongozi bora na mzuri siyo suala la jinsia bali ni uwezo wa mtu binafsi na kipawa na Karama aliyo jaaliwa na Mungu kiuongozi.

Lakini sote ni mashahidi wa namna lissu ambavyo alikuwa akimbagua Rais wetu kwa kusema huyu ni Mzanzibari na hana uchungu Taifa hili na kauli nyingine mbalimbali za kutweza utu wa Rais wetu. Sasa mtu wa aina hii na mwenye mawazo ya kibaguzi hataishia kumbagua Rais wetu tu ambaye anajua fika ni Mtanzania na mwenye haki zote za kitanzania.

Mdomo wa Lissu unanifanya nimchukue kwa sababu najua atafanya kazi ya kueneza chuki ,ubaguzi,fitina ,marumbano yasiyo na tija pamoja na kuhatarisha usalama wa Taifa letu. Kwa sababu yeye ni mtu ambaye akili yake anaijua Mwenyewe na inavyomuongoza.

Lakini mimi niseme tu kuwa ni aidha akubali njia ya maridhiano ambayo Mheshimiwa Mbowe alikuwa ameiongoza. Kwa sababu siasa za jino kwa jino hataziweza na itakuwa ni ngumu sana kuziendesha hapa Nchini. Ni siasa ambazo zimeumiza wengi,kuwaacha wengi na vilema,kuwafanya wengi kupoteza maisha,masomo,ajira ,kupoteza marafiki na hata wengine kupoteza kabisa muelekeo mpaka leo hii hususani kundi la vijana.

Hivyo asifikirie kuwa siasa za muundo huo na zenye misimamo mikali zitafanikiwa hapa Nchini. Hakuna anayeweza kuandamana mbele ya polisi ambao wamepiga marufuku jambo fulani kufanyika. na wala hakuna atakayekuwa tayari kuhatarisha usalama wake na Maisha yake barabarani. katika hilo namuhakikishia kuwa hatafanikiwa hata kidogo.

Isitoshe watanzania wa sasa wanatambua ya kuwa wapinzani wa Tanzania wanaongozwa na matumbo yao tu yaani uchumia tumbo tu. Kwa sasa upinzani hauaminiki hata kidogo kwa wananchi maana wanajua ni vigeugeu tu. kwa hiyo Lissu akitaka aendeshe siasa za kibabe basi ataishia kuumia tu. kwa sababu vyombo vyetu vya ulinzi hususani Jeshi la Polisi halitakuwa tayari kuona chama au mtu fulani anataka kuleta na kuchochea uasi hapa nchini.

CHADEMA wamepoteza chaguo sahihi na kuchagua mtu asiye stahili kuiongoza CHADEMA. Najua mnafuraha ya muda mfupi kwa baadhi yenu. Ila mtalia sana na kumkumbuka mbowe Mwamba na Jabali la siasa za upinzani hapa Nchini. Muda ni Mwalimu mzuri sana.

Ngoja tuupe muda nafasi ili uwapeni majibu . Siku yaja ambapo mtalia na kububujikwa na machozi ya huzuni na kumkumbuka sana Mbowe. Kazi iendelee, Mama Ametufikia na kuwafikia watanzania kwa utumishi wake uliotukuka wa kugusa Maisha ya watanzania wanyonge wasio na Sauti. Mama ANATOSHA kuendelea kuliongoza Taifa letu kwa muhula wa pili

KUMEKUCHA Makala MJASIRIAMALI JANUARI 23, 2025 9

# FREEMAN MBOWE HAKUSOMA ALAMA ZA NYAKATI

MIAKA 21 ya utawala wa Freeman Mbowe ndani ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo(CHADEMA) imehitimishwa na wajumbe wa Mkutano Mkuu kupitia uchaguzi Januari 21 mwaka huu.

Mbowe ameangushwa katika nafasi ya Uenyekiti na aliyekua Makamu wake Tundu Lissu ambaye ni kama alibebwa na upepo wa kisiasa wa mabadiliko ndani ya chama hicho.Maswali ni mengi juu ya kuangushwa kwa Mbowe.

Lissu na Mbowe, wote ni miamba ya Siasa za Upinzani Tanzania, huku Mbowe akiwa amedumu kwenye nafasi hiyo kwa takribani miongo miwili sasa.Lipo jicho la kisiasa linatazama kuangushwa kwa Mbowe na Makamu wake Lissu ni kama fedheha pengine angeweza kusoma upepo kuliko kusubiri kuangushwa kupitia sanduku la kura licha ya kuwa demokrasia imetumika kuamua.

Je, nini maoni ya Wanafalsafa, Wanazuoni, Wanasiasa, na Wapenzi na Wananchi wa Tanzania?.

Tumesikia mengi mpaka sasa. Sitasemea makundi yote hayo, nitajaribu tu kujikita katika Uchambuzi wa Kifalsafa, ambao unaweza kuangazia uwanda mpana zaidi hata kugusa makundi yote hayo. Hebu naomba tutafakari pamoja, uchambuzi huu ambao unatumia Fikra tunduizi (Critical Thinking):

NB: Kuanzia sasa,nitatumia maneno FAM,kumaanisha Freeman Aikael Mbowe.TAL, kumaanisha Tundu Antipas Lissu.CDM kumaanisha CHADEMA.CCM kumaanisha Chama Cha Mapinduzi.

Je,FAM alikua mwimbaji mzuri ambaye hakujua wakati sahihi wa kuondoka jukwaani, au TAL naye ni mwimbaji mzuri ambaye hakujua wakati sahihi wa kuingia jukwaani? Ni nani kati yao anachelewa kutoka,kuingia? Kichokoo hiki kinachobeba kichwa cha habari cha uchambuzi huu wa Kifalsafa, kituongoze katika tafakari hii. Na hapa, makundi kadhaa, kama nilivyosema awali,yamejitokeza kutia neno.

Wapo watu wanaoona kwamba, FAM ni mwimbaji mzuri aliyechelewa kutoka, wakirejea kazi nzuri alizofanya kwa miongo kadhaa.CDM chini ya mikono yake, imeweza kuenea nchi nzima, na kutekeleza operesheni kadhaa zilizokimarisha chama na hata kuwa tishio dhidi ya vyama vingine vya Siasa hasa CCM.

Kama ilivyo kawaida ya Duniani, vitu vikubwa vinakuwa viwili viwili ili kubalansi mizania, yaani mfano Mungu na Shetani, jinsia KE na Me, Usiku na Mchana, Juu na Chini, Cocacola na Pepsi, Iphone na Samsung, Ukristo na Uislam, Simba na Yanga nk., ndivyo CCM na CDM zinavyotazamwa katika ushindani.

Kundi hili liliona kuwa FAM anapaswa kupumzika kwa heshima ili afaidi kazi yake njema aliyoifanya. Lakini hapa pana shaka kidogo, unafikiri kundi hili liliona tu FAM apumzike kwa sababu hiyo tu? La hasha! Walikua na ajenda nyingine nyuma yake kwamba 'Intergrity' ya FAM, imeingia doa, ya kile kinachodaiwa kwamba amekua mshiriki wa Siasa 'dangayifu' za CCM ili kudhoofisha safari ya CDM kushika Dola.

Katika dhana hii, inapunguzwa makali na hoja kwamba FAM ni mpole na mwenye busara sana, na hivi anasikiliza au kama wasemavyo vijana wa mjini—anapigiga 'sound'/anaongeleka.

Kundi hili lilirejea sakata la maridhiano yaliyofeli kwa baadhi ya mambo, kutosimamisha wagombea wa kutosha wa Uchaguzi uliopita, madhila mbalimbali ya Wanachama na Viongozi wa CDM na misimamo ya kutotumia nguvu ya Umma katika kusonga mbele.

Hapa ndipo Rais Samia anapoingia kwenye hili sakata la miamba hii miwili, kwani mara baada ya Mama huyu kushika Madaraka ya Rais, alifanya jitihada za kuifungua nchi na hivi akaja na R4 yaani 4R, ambazo zikawa ndio moja kati ya msingi wa maridhiano, na kusaidia kesi kadhaa za Wanachama wa CDM ikiwemo TAL kufutwa, kufutwa kwa tangazo haramu la mikutano ya hadhara, kuwapa upinzani ruzuku, kubadili sheria ya Uchaguzi na Tume, nk.

Ingawa katika hayo bado baadhi ya Wana CDM hawakuyaunga mkono, akiwemo TAL aliyepinga mara kadhaa kuhusu maridhiano. Hapa FAM alionekana kuwa mshirika mzuri wa CCM, na hivi baadhi ya watu kutomuamini.

Lakini pia wengine wakahoji, kwani yalikuwa ni maridhiano ya nini? Ya nani? Dhidi ya nani na nani? Na sisi wengine tunahoji, ni kwanini maridhiano (kama yalikuwepo) yalivunjika?? majibu watakuanayo wanasiasa.

TAL, Mwanasiasa mwenye msimamo mkali wa kati, mthubutu na asiyeonea jambo soni, rekodi yake ipo wazi, akaibua sakata la rushwa kwenye Chaguzi za ndani ya CDM, akatangaza juu ya 'Mapesa' aliyowahi kupelekewa ili ahongwe.

Alijaribu kuwataja baadhi (mmoja) hadharani kuwa ndiye aliyefanya hiyo konekesheni, na kwamba 'mapesa' hayo yamewavuruga kweli! Bado swali likabaki, ni nani aliyeruhusu fedha hizo kumwagwa ndani ya chama, zikisadikika kutokea upande wa pili?

Pia kundi hili hudhani kuwa uwezo binafsi wa fedha wa FAM unatumika kutokuwa na uwazi wa dhati na fedha za chama. Hivyo wanahisi kuna harufu ya 'upigaji.'

Hoja dhidi ya TAL, zinahusu aina yake ya Siasa yenye ukali na isiyo na simile.Yaani siasa za heka heka na mtiti mtiti kwamba kama alivyosema mwenyewe wakati akihojiwa, 'Siasa za heavy duty machine', Siasa za nginja nginja!Aina hii ya Siasa inaonekana kukosa busara na kwamba akiwa Mwenyekiti, italeta fujo?

Swali la Kifalsafa ni kwanini TAL alibadili gia angani, (kama alivyofanya FAM) kipindi cha Uchaguzi wa 2015, kwa kumleta hayati Mh. Lowassa kugombea Urais CDM, kwa kuamua kugombea Uenyekiti Taifa, ilihali alishatangaza kugombea Umakamu??

Ni nini kilimsukuma? Au ndio ataleta fujo na uvunjifu wa amani kama baadhi wanavyodai? Au atakua mkombozi kwa wale wanaoteseka kwa yale ambayo huwa anayapigania?

Je, ni nani atakua mgombea Urais wa CDM 2025? CDM inamuandaa FAM baada ya kutokugombea au kugombea na kukosa Uenyekitu au TAL, baada ya kugombea na kupata au kukosa Uenyekiti?Je, CDM itabaki salama kama FAM akiamua kugombea pia? Au itasambaratika kama ilivyowahi kutokea kwa CUF imara na TLP?.

Haya ya pili yakitokea, je, imani kwa Wananchi juu ya vyama vya Siasa itabaki vile vile au? Vipi kuhusu CCM inayodhaniwa kuwa nyuma ya saga hili? Je, inafurahia hali hii au inachukizwa?

Au imetulia pembeni, kama Bondia machachari anayejisemea kimoyomoyo "Nyie gombaneni mnavyoweza, mkishakubaliana juu ya bondia wenu wakupambana na mimi, basi mleteni nimbonde Kichama na Ki-Uchaguzi".

Lakini hapa kuna mtego mkali….!

Kama FAM ataamua kutokugombea, ina maana anakubaliana na Shutuma zote dhidi yake zilizotolewa na TAL na zinazosemwa na baadhi ya Wanachama na Wapenzi?.

Na kama akikataa,ina maana atakua amekubali pia kuwa anasapotiwa na mahasimu wa CDM ili wasishike Dola na kwamba anakomaa kwakua ananufaika na Upigaji?.

Ni nini kitabadilika katika Siasa za Tanzania nje ya CDM? Unaonaje, ni rahisi kiasi kwa TAL kuwa Mwenyekiti wa CDM Taifa, kuliko kuwa Mgombea Rais wa Tanzania? Au ni Ngumu kiasi gani kwa TAL/FAM kuwa Mgombea Urais wa Tanzania kuliko kuwa Mwenyekiti wa Taifa?

Kama FAM angekubali kutokugombea na kukubali kubeba lawama zote hizo dhidi yake; basi kweli angekua ni Baba wa Siasa za Upinzani Tanzania. Maana atakua hajakipasua Chama na amemuhifadhi TAL chamani. Maana nionavyo mimi wote wanahitajiana kutokana na tofauti ya Character zao Kisiasa.



**MAONI YA MWANDISHI**

Siasa ni kama Mawimbi ya bahari, sometimes yanatulia na sometimes yanatibuka. Yanapotulia, anahitajika nahodha mtulivu mpole, pale yanapotibuka, anahitajika nahodha Machachari na mdhubutu…..swali, je, mawimbi ya bahari yametibuka? Je, mawimbi ya bahari yametulia?

Anahitajika nahodha wa namna gani? Katika hili CDM wanapaswa kutazama asili ya hasimu wake kisiasa, kwani si vyema kutoa panga alani, ilihali hasimu wako amekuja kwa amani.Aliimba Selemani Msindi—Afande Sele na Philipo Nyandindi—O Ten mtoto wa Kola Hill Morogoro)

Sisi wapenda Demokrasia tunatamani kuona wakionesha dhana hiyo, kufanya siasa za Demokrasia na Maendeleo. Wahenga walisema, Mwimbaji mzuri hujua muda muafaka wa yeye kushuka jukwaani (kabla hajaboa watazamaji).

Anguko la Mbowe limechangiwa na kutosoma alama za nyakati mahitaji ya wanachama mtaani nini hali ambayo iliwafanya wajumbe kufuata hisia za wanachama wa kawaida wanamuhitaji nani.

Tchao.!

**Dr. Apiov S. Lwiwa, PhD**
Ni Daktari wa Falsafa katika Falsafa
Mchambuzi na Mtafiti wa mambo ya Kijamii na Maendeleo
Barua Pepe: apiovlwiwa@gmail.com

# CHADEMA YA TUNDU LISSU ITAKUWA YA AINA GANI?

**BBC,**

**HATIMAYE lile ambalo lilikuwa likingojewa kwa muda mrefu sasa limekamilika,Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema),kimepata Mwenyekiti mpya, Tundu Antiphas Mughwai Lissu aliyeshinda kwa kura 513 (51.5%), dhidi ya Freeman Aikaeli Mbowe aliyepata kura 482 (48.3%)**

Ni baada ya miaka takribani 20 ya uongozi wa Freeman Aikaeli Mbowe, aliyechukua hatamu za kuwa Mwenyekiti wa Chadema tangu 2003. Hata mpinzani wake katika uchaguzi huu Tundu Lissu, amekiri, kukuwa kwa Chadema kunatokana na kazi kubwa iliyofanywa na Mbowe.

Bila shaka ni jambo la kushukuru kwa wafuasi wa Chadema kwamba kamera za vyombo vya habari hazijanasa matukio ya watu wakishika vikosi katika uchaguzi huu; kwa jinsi ushindani, malumbano na maneno yalivyokuwa mengi, hatimaye uchaguzi umekwenda vyema, na Freeman Mbowe amekubali kushindwa na kumpongeza Lissu, ni kiashiria cha ukomavu wa kisiasa.

Kupitia Chadema, Lissu ameshika nyadhifa nyingi; ikiwemo Mbunge wa Singida Mashariki, Mwanasheria Mkuu wa chama hicho, Mnadhimu Mkuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Makamu mwenyekiti wa Chadema upande wa Bara, na sasa ni Mwenyekiti.

Kama ilivyo kwa ushindi wowote, kwanza ni furaha lakini kisha, ni kukabiliana na majukumu ya kiuongozi. Swali ambalo wengi sasa wanajiuliza: Je, Lissu atailetea nini Chadema? Pia atakabiliana vipi na changamoto zijazo na zile ambazo tayari ziko mbele yake?

**Maridhiano ndani ya chama**

Akizungumza katika mkutano mkuu jana, Lissu amesema "nimekaa na mwenyekiti (Mbowe) kwa zaidi ya miaka 20, hatujawahi kugombana, hatujawahi kukosana. Ndio tumetofautiana misimamo, lakini hatujawahi kugombana na hili litaendelea baada ya leo."

Lakini ndiye Lissu huyo huyo ambaye katika mahojiano ya BBC Swahili, alipoulizwa kuhusu uhusiano wake na Mbowe alisema. "Tukikutana hivi, hatupigani ngumi. Lakini uhusiano haupo kama mwanzoni."

Pia akarusha mawe kwa Mbowe kwa kusema, "kugombea kwangu namuokoa Mbowe, namsaidia Mwenyekiti Mbowe kulinda urithi wake. Kuna hatari ya kutoka kuwa Mugabe 'mpigania uhuru' na kuwa 'Mugabe dikteta, rais wa maisha.' Haipaswi kuondoka kwenye madaraka kwa kukufukuzwa kwa sababu ya watu wamekuchoka."

Kauli hizi zilitoa ishara kuwa mambo kati ya watu hawa wawili hayakuwa sawa katika kipindi cha kuelekea uchaguzi wa kumsaka mwenyekiti, na hivyo juhudi za makusudi za kuurudisha uhusiano uliotetereka, hazina budi kufanyika kwa faida ya chama.

Vilevile, Mbowe ana wafuasi wengi na bado ushawishi wake ni mkubwa ndani ya Chadema, ana kundi kubwa la watu wanaomuunga mkono, ndio maana hata katika uchaguzi huu, hakupata kura sifuri, kura alizopata ni kielelezo tosha juu ya ukubwa wa jina lake ndani ya chama.

Mbowe pia ameeleza wazi kuwa Chadema imeachwa na majeraha makubwa kutokana namna kampeni za uchaguzi huo zilivyoendeshwa na amemtaka Lissu na viongozi wengine wapya kuleta maridhiano.

Kwa kuzingatia hilo, Lissu kama Mwenyekiti atakuwa na kazi ya kuyaleta pamoja makundi haya mawili, yaani kundi lake na lile na Mbowe. Na kuhakikisha Mbowe na wafuasi wake wanaendelea kutoa mchango wao wa hali na mali katika kuendesha shughuli za chama hicho.

Mpasuko ndani ya chama hudhoofisha chama chochote kile kinachotaka wafuasi wengi wa kukipigia kura na kupata ushindi katika chaguzi.

**Atapambana vipi na rushwa?**

Januari 17 mwaka huu wakati akizungumza katika mdahalo wa kisiasa, Tundu Lissu alisema, "mimi ndiye niliyekuwa wa kwanza, kupuliza filimbi kwamba kuna rushwa kwenye chaguzi zetu (Chadema). Tuna tatizo. Muda huu tunapozungumza, kuna wajumbe wanasafirishwa, wanawekwa kwenye mahoteli, makambi, wanapewa pesa, wanalishwa na wagombea. Kuna uchafuzi wa aina hiyo, unoafanywa na wagombea na wapambe wao."

Hili ni tatizo ambalo wakati fulani huko nyuma lilizungumzwa pia. Mwezi Mei 2020, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Tanzania (Takukuru), ilitangaza kuanzisha uchunguzi kuhusu tuhuma za matumizi mabaya ya fedha ndani ya Chadema.

Aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Takukuru, Brigedia Jenerali John Mbungo alieleza, "kwa mujibu wa taarifa tulizo nazo, kuna matumizi mabaya ya fedha za michango ya wanachama, ambayo kwa mujibu wa katiba yao wanadai imeanishwa wachangie. Lakini, matumizi yake ndio yanatilia mashaka, kuna fedha nyingi zinatumika ndivyo sivyo, nje ya makubaliano yao. Kwa hiyo, tunachunguza matumizi yasiyo sahihi ya fedha zao."

Ikiwa ufisadi ama rushwa ni tatizo ambalo lipo ndani ya Chadema na lipo kwa muda mrefu, ni matarajio ya wengi kwamba hii itakuwa ni kazi nyingine kubwa ambayo Lissu inamngoja mbele yake.

**Uhusiano wa upinzani na serikali**

Moja ya hoja ambayo Lissu ameitumia kumkosoa Mbowe, ni namna alivyokuwa akiendesha siasa zake na serikali. Kwa lugha nyingine, Lissu alimwona Mbowe amekuwa laini mbele ya chama tawala na serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan.

"Mwenyekiti aliyekwenda gerezani, si mwenyekiti aliyetoka gerezani miezi minane baadaye. Yule aliyetoka gerezani alikuwa tofauti, akiimba maridhiano anaimba mapendano," alisema Lissu.

Alipoulizwa na BBC juu ya mwelekeo wake mpya wa kisiasa na utakuwa na tofauti gani na hali ya sasa. Tundu Lissu amesema:

"Ni mwelekeo wa harakati za mapambano ya demokrasia, hakuna tena kuimbiana habari ya maridhiano yasiyokuwepo, hakuna habari ya kualikana kuzungumza mambo yasiyojulikana. Nia mapambano ya kudai mabadiliko. Na zitakuwa ni siasa za mshike mshike kweli kweli. Ndio historia ya mapambano ya kidemokrasia ilivyo dunia nzima."

Chadema kama vilivyo vyama vingine vya upinzani, inapigia upatu kuwepo kwa katiba mpya, tume huru ya uchaguzi, inataka uchaguzi huru na haki mwishoni mwa mwaka huu, bila ya wagombea wao kuenguliwa bila sababu za maan, pia inataka viongozi na wafuasi wake wasibughudhiwe na vyombo vya dola wanapokuwa kwenye shughuli zao za kisiasa.

Katika nchi yenye demokrasia inayoeleweka, yumkini hayo sio mambo ambayo utawala unapaswa kuyatoa kama huruma kwa vyama vya siasa, ni mambo ambayo yapo kikatiba na kisheria, bahati mbaya utawala nchini Tanzania – kama ilivyo kwa tawala nyingine nyingi duniani – hautendi haki wakati wote. Kuna nyakati za vuta ni kuvute, pingu kiunoni na kirungu mkononi.

Maswali yanayoibuka kwa muktadha huo:Je,Chadema chini ya Lissu itahitaji kuwa na uhusiano au ushirikiano na utawala ili kuyafanikisha hayo? Au ina uwezo wa kuyafanikisha bila ya mwingiliano wowote na upande wa serikali?

Lissu baada ya kuibuka na ushindi alianza hotuba yake kwa kusema, atazungumza kwa kuchagua maneno yake kwa uangalifu, na kweli akafanya hivyo. Je,tutarajie Lissu ambaye ataendelea kuchagua kauli zake hata akiwa katika harakati dhidi ya chama tawala na serikali yake?

Bila shaka, Lissu kwa sasa ndiye mmiliki wa jawabu ya maswali haya yote.





# NCHIMBI MGOMBEA MWENZA SAHIHI KATIKA NYAKATI SAHIHI




Na Lucas Hebel Mwashambwa

**DK.EMMANUEL Nchimbi ndiye Mgombea mwenza wa Rais Dk.Samia Suluhu Hassan kuelekea uchaguzi Mkuu utakaofanyika Oktoba mwaka huu.Nchimbi ambaye ni Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi(CCM)alipitishwa na Mkutano Mkuu wa Chama hicho kule jijini Dodoma wiki iliyopita akichukua nafasi ya Dk.Philip Mpango aliyeomba kupumzika.**

Kwangu CCM imepata mgombea sahihi katika nyakati sahihi.Jambo muhimu kwanza la kuzingatia katika mambo ambayo CCM huwa makini na haiwezi kufanya mzaha au majaribio au kukosea basi ni katika suala zima la kusuka safu nzima ya uongozi wake ndani ya chama.

Uteuzi wa Dk.Nchimbi katika nafasi y mgombea mwenza ni matokeo ya upembuzi yakinifu wa chama hicho.CCM hufanya hivyo sababu inatambua kuwa yenyewe ndiyo moyo wa Nchi,ndio itaoyo Dira na muelekeo wa Taifa letu katika kuisimamia serikali.

Inajuwa kuwa CCM ikiwa dhaifu na legelege ni lazima serikali iyumbe na kukosa muelekeo pamoja na kulitikisa Taifa.Ndio maana ukiangalia safu yake ya uongozi hushikwa na kuongozwa na watu makini, watulivu, hodari, majasiri, Wazalendo na wenye uzoefu wa kutosha kiuongozi.

Kwa hakika na kiukweli Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi ni kiongozi makini, hodari,shupavu, madhubuti na imara kwelikweli.Ni kiongozi mwenye uwezo mkubwa sana wa kujenga hoja,kutetea hoja,kufafanua na kuichambua hoja kwa utulivu ,umakini na uhodari wa hali ya juu sana.

Hana mihemuko wala jazba wala ukurupukaji.Ni msikivu sana katika kusikiliza hoja Kabla ya kufungua kinywa chake na kujibu au kutoa ufafanuzi au maelezo.

Hii ndio sababu ya kushuhudia CCM ikiendelea kuwa chama chenye nguvu,ushawishi ndani na nje ya mipaka ya Tanzania pamoja na kuendelea kuaminika ,kuungwa mkono na kukubalika kwa watanzania.ndio sababu ya kushuhudia nidhamu ikitawala na kutamalaki ndani ya chama.

Maana ikumbukwe chama ambacho ndani yake hakuna nidhamu wala kuheshimu misingi ,kanuni ,taratibu ,sheria na katiba ya chama ni ngumu sana chama hicho kupata ushindi na kuimarika.Hata Jeshi ambalo askari wake hawana nidhamu ni ngumu sana kushinda vita ya aina yoyote ile.

Lakini tunamshuhudia Balozi Dkt Emmanueli Nchimbi namna ambavyo amekuwa mlezi wa jumuiya zote na kuzifanya kuendelea kuimarika na kuwa zenye nguvu lakini pia tumeona namna ambavyo amekua akikemea na kumkemea yeyote yule atakayeonekana kukichafua chama kwa kauli au maneno au matendo yake hadharani.

Kwa hakika Balozi Dkt Emmanueli Nchimbi alikuwa chaguo na pendekezo sahihi kabisa la kushika nafasi ya ukatibu Mkuu wa CCM. Kwa sababu ni kiongozi mwenye misimamo,uadilifu,utulivu, unyenyekevu,usikivu,uzoefu wa kiuongozi ndani ya chama na serikalini pamoja na kuwa mtu mwenye hofu ya Mungu na kwa hakika anaendelea kukiheshimisha sana chama cha Mapinduzi kwa watanzania.

Ndiyo maana amekuwa akikemea sana hadharani Vitendo vyote vyenye kukiuka maadili na kwenda kinyume na misingi ya kidemokrasia. Kwa ufupi ni kuwa Balozi Dk.Emmanuel Nchimbi ni mtu Mwema,muungwana, mpenda haki ,mwenye moyo wa huruma ,mwana demokrasia wa kweli na mzalendo kwelikweli.

Ni hazina kwa chama Na Taifa letu kwa ujumla wake.Kazi iendelee, Mama Ametufikia na kuwafikia watanzania kwa utumishi wake uliotukuka wa kugusa maisha ya watanzania wanyonge wasio na Sauti.Mama ANATOSHA kuendelea kuliongoza Taifa letu kwa muhula wa pili.

# USIYOYAJUA KUHUSU BALOZI DK.EMMANUEL NCHIMBI

NA MWANDISHI WETU,

CHAMA cha Mapinduzi(CCM) kimekamilisha mchakato wa kupata mgombea wake Urais wake+` kupitia uchaguzi Mkuu utakaofanyika Oktoba mwaka huu.

Mkutano Mkuu Maalumu wa CCM uliofanyika Januari 18-19 kule jijini Dodoma mbali na kumuidhinisha Steven Wasira kuwa Makamu Mwenyekiti wa chama hicho lakini ulimpitisha kwa kishindo Rais Samia Suluhu Hassan kuwa mgombea Urais huku pia jina la Balozi Dk.Emmanuel Nchimbi likichomoza kama Mgombea mwenza.

Nchimbi aliidhinishwa kuchukua nafasi hiyo kufuatia uamuzi wa Makamu wa Rais Dk.Philip Mpango kumuandia barua Rais Samia kwamba anaomba

kupumzika na sasa mikoba ya mgombea mwenza imekabidhiwa kwake.

**Balozi Nchimbi ninani?**

Jina la Balozi Dk.Emmanuel John Nchimbi sio jina geni kwenye anga la siasa za Tanzania.Ni moja ya wanasiasa wakubwa, mahiri na wakongwe wanaoendelea kuteka uga huu wa siasa za Tanzania.

Balozi Dk.Emmanuel John Nchimbi ni moja ya wanasiasa wakubwa sana kwenye siasa za Tanzania.Kwa utumishi na uzoefu wake mkubwa ndani ya CCM na serikali akiwa na zaidi ya miaka 35 akishika nafasi kubwa na nyeti za maamuzi.

**Ndiye Katibu Mkuu wa CCM**

Ameshika nafasi mbalimbali kwenye ngazi za chini na za msingi za CCM,akiwa Chuo mwaka 1997 alichaguliwa kuwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM (NEC)na mwaka mmoja mbele 1998,alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) Jumuiya aliyoiongoza mpaka mwaka 2008.

Pia amewahi kuwa Mkuu wa Wilaya ya Bunda iliyoko mkoani Mara wakati wakati wa Awamu ya 3 ya Hayati Benjamin Mkapa kuanzia mwaka 2003 hadi 2005.

Kuwa Kiongozi Mkuu wa Jumuiya hiyo ya Vijana kwa ngazi ya Taifa, moja kwa moja kukampa tiketi ya kuwa Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM na Halmashauri Kuu (CC & NEC).

Kamati Kuu na Halmashauri Kuu ya CCM ni moja ya vikao vya juu kabisa vitatu vya CCM kando ya Mkutano Mkuu wa CCM Taifa ambavyo vinafanya maamuzi makubwa ndani ya Chama hicho ikiwemo kumpitisha Mgombea Urais wa CCM, Mwenza,Wabunge lakini vikiwa ni vikao vinavyojadili hali ya CCM na utekelezaji wa Ilani yake na serikali na mengine mengi makubwa yanayogusa maslahi ya Taifa zima.

Baada ya kuhudumu kwenye nafasi kubwa ndani ya Chama na zenye maamuzi makubwa ndani ya Chama na Taifa,



Mwaka 2005 Dkt. Nchimbi aligombea Ubunge kwenye Jimbo la Songea Mjini na kushinda ambapo moja kwa moja Rais wa Awamu ya 4 wa kipindi hicho Dkt.

Jakaya Kikwete alimteua kuwa Naibu Waziri kwenye Wizara 3 akianza kuwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo kuanzia Januari 2006, kisha Naibu Waziri wa Kazi, Ajira na Vijana mwaka huohuo Oktoba pamoja na Naibu Waziri wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa alikohudumu kuanzia Februari 2008 hadi 2010 kwenye Uchaguzi Mkuu.

Mwaka 2010 aligombea tena na kushinda na hapo sasa Rais wa Awamu ya 4 Dkt. Jakaya Kikwete akamteua kuwa Waziri kamili akianza kuwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo na baadae Waziri wa Mambo ya Ndani.

Mwaka 2016, Dk. Nchimbi aliteuliwa na Aliyekuwa Rais wa Awamu ya 5 Hayati John Magufuli kuwa Balozi wa Tanzania nchini Brazil kabla ya baadae mwaka 2022 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt.

Samia Suluhu Hassan kumbadilishia Kituo cha kazi ya Ubalozi kwa kumteua kuwa Balozi wa Tanzania nchini Misri, nafasi aliyohudumu mpaka mwaka Jana 2023 alipomaliza muda wake na kurudi nchini kwa mujibu wa sheria.

Baada ya kazi kubwa akianzia ngazi za chini za uongozi, Uenyekiti wa Jumuiya ya Vijana Taifa (UVCCM), Mbunge, Naibu Waziri hadi Waziri kamili na Ubalozi hatimaye Januari 15, 2024 Dkt. Nchimbi aliteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa CCM, Mtendaji Mkuu wa Chama hiki kinachoongoza Taifa letu Tanzania

Anasifika kwa misimamo madhubuti isiyoyumba (hili nitalichambua) akiwa na ushawishi mkubwa ndani ya Chama na Nje hasa kwa kufanya kazi ndani na Nje ya Nchi.Kwa CV yake hii ilivyoshiba akishika nafasi kubwa na nyeti akianzia ngazi za chini, ni mtu madhubuti kuweza kuwa msaidizi namba moja wa Mkuu wa Nchi.

Ni ukweli usiopingika kwamba kwa Rais kariba ya Dk. Samia anayefanya mageuzi makubwa ya maendeleo ndani ya nchi anahitaji kuwa na wabobezi wakubwa wa siasa na utumishi kumsaidia kutafsiri maono yake.

Balozi Nchimbi ni Msomi mzuri aliyebobea kwenye masuala ya Fedha na Benki akihitimu Shahada ya Uzamivu (PHD) kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe mwaka 2011.



# Athari za Trump kuiondoa Marekani katika Shirika la Afya Duniani WHO

BBC

**RAIS wa Marekani Donald Trump ametia saini amri ya kuanza mchakato wa kuiondoa Marekani kuwa mwanachama wa Shirika la Afya Duniani (WHO).**



"Hili ni jambo kubwa," rais mpya wa Marekani aliyeapishwa alisema alipokuwa akiidhinisha hati hiyo baada ya kurejea tena katika Ikulu ya Marekani.

Ilikuwa ni moja ya amri kadhaa za utendaji alizotia saini siku ya kwanza madarakani.Hatahivyo uamuzi wake huenda sio tu ukaathiri utandekazi wa shirika hilo la Afya bali hata huduma zake kote duniani.

Kulingana na taarifa za matumizi ya fedha za hivi karibuni zilizotolewa na WHO, Marekani ndio mfadhili mkubwa wa shirika hilo.Je, ni kwanini Trump ameamua kuchukua uamuzi huu?

Hii ni mara ya pili kwa Trump kuamuru Marekani kujiondoa kuwa mwanachama wa WHO.Trump alikosoa jinsi shirika hilo la kimataifa lilivyoshughulikia janga la Covid-19 na kuanza mchakato wa kujiondoa kutoka kwa taasisi hiyo ya Geneva wakati wa janga hilo.Rais Joe Biden baadaye alibatilisha uamuzi huo.

Agizo hilo lilisema Marekani inajiondoa "kwa sababu ya WHO kutoshughulikia janga la Covid-19 ambalo liliibuka Wuhan, China, na majanga mengine ya afya ya ulimwengu, kushindwa kwake kupitisha mageuzi yanayohitajika haraka, na kutokuwa na uwezo wa kuonyesha uhuru kutoka kwa yasiyofaa. ushawishi wa kisiasa wa nchi wanachama wa WHO".

Amri hiyo ya utendaji pia ilisema hatua hiyo ilitokana na "malipo yasiyofaa" ambayo Marekani ilitoa kwa WHO, ambayo ni sehemu ya Umoja wa Mataifa. Trump alipokuwa ofisini kwa mara ya kwanza alikosoa shirika hilo kwa "kuipendelea China" katika kukabiliana na janga la Covid-19.

Aliishutumu WHO kwa kuegemea China kwa jinsi ilivyotoa mwongozo wakati wa mlipuko huo.Mwaka 2020 wakati wa janga la Covid Tramp alisema: "Ikiwa WHO ingekuwa imefanya kazi yake ya kutuma wataalamu wa kitabibu nchini China ili kutathmini hali ilivyo, na kuikosoa China kwa kutokuwa wazi, ugonjwa huo ungeweza kudhibitiwa na kutokea kwa idadi ndogo ya vifo."

WHO imekuwa ikifadhiliwa vipi?

Shirika hilo liliundwa 1948 kama sehemu ya mfumo wa Umoja wa Mataifa, likilenga kuendeleza afya bora, kuhakikisha dunia inakuwa salama na kuhudumia wale walio katika hatari zaidi."Taasisi hiyo, ambayo makao yake makuu ni Geneva (Uswizi), imekuwa ikipata Ufadhili wa lazima na ule wa kujitolea

Kwanza, kuna pesa ambazo ni lazima zitolewe na nchi washirika 194.

Kila nchi inatakiwa kulipa kiwango fulani kulingana na Umoja wa Mataifa kupitia mfumo ambao ni vigumu kuelezeka kwasababu unazingatia utajiri wa nchi na idadi ya watu.Ni pesa ambayo kwa msingi huwa inasimamia mishahara na utawala wa shirika hilo.

Pili ni ufadhili wa kujitolea unaowezesha nchi na maeneo kuahidi pesa watakazochangia kwa maswala maalum, kama vile chanjo ya ugonjwa wa polio, afya ya wanawake au ukabilianaji na matumizi ya tumbaku.

Marekani ilichangia dola za Marekani bilioni 1.284 katika kipindi cha 2022-2023, kuwezesha WHO, Marekani na nchi nyingine na washirika kutambua na kukabiliana na dharura, kuzuia vitisho vya magonjwa kuenea katika mipaka na kuendeleza vipaumbele vingine muhimu vya afya duniani.

WHO ilipokea dola za Marekani milioni 363 kama fedha za ufadhili kipindi cha 2022-2023 kulingana na taarifa katika wavuti wa shirika hilo.

Hatahivyo idadi ya wafadhili imendeelea kuongezeka huku mataifa kama vile , Ujerumani, Tume ya Ulaya, Norway, Jamhuri ya Korea zikijiunga na Marekani , Luxembourg, India na Uhispania katika kulifadhili shirika hilo.Baada ya Marekani, ni shirika la kibinafsi la Bill and Melinda Gates Foundation, ambalo hutoa ufadhili mkubwa kupitia hazina ya the Global Fund

Mchangiaji mkubwa wa tatu ni GAVI, shirika ambalo linajumuisha mashirika ya umma na serikali ambayo yanapigia upato kuongeza upatikanaji wa chanjo kwa nchi 73 katika maeneo ya kaskazini kote duniani.

**Athari ya kuondolewa kwa ufadhili wa Marekani**

Ikiwa Marekani itafanikiwa kuondoa mchango wake , WHO itakuwa na changamoto."Uamuzi wa Trump kusitisha ufadhili kwa WHO utakuwa na athari kubwa", Jack Chow, aliyekuwa balozi wa Marekani katika kukabiliana na ukimwi na aliyekuwa Naibu Mkurugenzi wa WHO alisema mwaka 2020 wakati Marekani ilipojaribu kuchukua hatua kama hiyo.

"Hili linasababisha matatizo kwasababu ni wafadhili ndio wanaoandaa ajenda zitakazofuatwa na shirika hilo badala ya kufanya maamuzi yao kwa kuzingatia taaluma," Chow amesema katika mahojiano na BBC Mundo.

**.Chanzo cha picha,Getty Images**

Maelezo ya picha,Mpango wa polio wa WHO unafadhiliwa kwa gharama ya juu duniani.

# WANAWAKE WA SUDAN WANAVYOKABILIWA NA UBAKAJI NA UNYANYASAJI NCHINI LIBYA



**BBC**

**"Tunaishi kwa hofu,"Layla anasema kwa njia ya simu kwa sauti ya kunong'oneza ili mtu asimsikie .Alitoroka Sudan na mumewe na watoto sita mapema mwaka jana kutafuta usalama na sasa yuko Libya.**

Kama ilivyo kwa wanawake wote wa Sudan ambao BBC ilizungumza nao kuhusu uzoefu wao wa kusafirishwa kwenda Libya, jina lake limebadilishwa ili kulinda utambulisho wake.

Kwa sauti ya kutetemeka anaelezea jinsi nyumba yake huko Omdurman ilivyovamiwa wakati wa vita vya wenyewe kwa wenyewe vya Sudan, ambavyo vilizuka mnamo 2023.

Familia hiyo ilikwenda Misri kwanza baada ya kuwalipa wasafirishaji dola 350 (£338) kuwapeleka Libya, ambako waliambiwa maisha yatakuwa bora na wataweza kupata kazi za usafi na hoteli lakini mara baada ya kuvuka mpaka, Layla anasema wasafirishaji waliwashikilia mateka, kuwapiga na kudai pesa zaidi.

"Ilibidi mwanangu atibiwe baada ya kupigwa mara kwa mara usoni," aliiambia BBC.Wasafirishaji hao waliwaachia huru baada ya siku tatu, bila kusema ni kwa nini. Layla alidhani maisha yake mapya nchini Libya yameanza kuwa mazuri baada ya familia hiyo kufanikiwa kusafiri magharibi na kukodi chumba na kuanza kufanya kazi.

Lakini siku moja mume wake aliondoka kwenda kutafuta kazi na hakurudi tena. Kisha binti yake wa miaka 19 alibakwa na mwanamume anayejulikana kwa familia kupitia kazi ya Layla.

"Alimwambia binti yangu kuwa angembaka dada yake mdogo ikiwa angezungumza juu ya kile alichomfanyia," Layla anasema. Anazungumza kwa sauti ya kutetemeka akihofia familia itafukuzwa mwanamke mwenye nyumba alikopangisha atasikia anachokisema.

Layla anasema kwa sasa wamekwama nchini Libya: hawana pesa za kuwalipa wasafirishaji wa watu kuondoka na hawawezi kurudi katika Sudan iliyokumbwa na vita.

"Hatuna chakula cha kutosha," anasema, akiongeza kuwa watoto wake hawaendi shuleni. "Mwanangu anaogopa kuondoka nyumbani kwani watoto wengine mara nyingi humpiga na kumtusi kwa kuwa mweusi. Nahisi ni kama nitarukwa na akili."

Wakimbizi wengi wa Sudan walikimbilia Misri wakati mzozo ulipozuka Aprili 2023 kabla ya kuvuka mpaka kuingia Libya.Mamilioni ya watu wameikimbia Sudan tangu vita kati ya jeshi na vikosi vya kijeshi vya Rapid Support Forces (RSF) vilipozuka mwaka 2023.

Pande hizo mbili kwa pamoja zilifanya mapinduzi mwaka 2021, lakini mapambano ya kuwania madaraka kati ya makamanda wao yaliitumbukiza nchi hiyo katika vita vya wenyewe kwa wenyewe.

Zaidi ya watu milioni 12 wamelazimika kuyakimbia makaazi yao, wakati njaa imesambaa katika maeneo matano, huku watu milioni 24.6, ikiwa ni karibu nusu ya idadi ya watu - wanahitaji msaada wa haraka wa chakula, wataalamu wanasema.Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia wakimbizi UNHCR limesema zaidi ya wakimbizi 210,000 wa Sudan sasa wako nchini Libya.

BBC imezungumza na familia tano za Wasudan ambao awali walikwenda Misri, ambako walisema walikabiliwa na ubaguzi wa rangi na vurugu, kabla ya kuhamia Libya, wakiamini kuwa itakuwa salama na fursa bora za kazi. Tuliwasiliana nao kupitia mtafiti katika masuala ya uhamiaji na kutafuta hifadhi nchini Libya.

Salma ameiambia BBC kuwa tayari alikuwa akiishi mjini Cairo, Misri, akiwa na mume wake na watoto watatu wakati vita vya wenyewe kwa wenyewe vya Sudan vilipozuka, lakini wakati idadi kubwa ya wakimbizi walipoingia nchini humo, hali ya wahamiaji nchini humo ilizidi kuwa mbaya.

Waliamua kuhamia Libya, lakini kilichokuwa kinawasubiri kilikuwa ni "jahanamu halisi", Salma anasema. Anaelezea jinsi, mara tu walipovuka mpaka, walivyowekwa katika ghala linaloendeshwa na wasafirishaji wa binadamu. Wanaume hao walitaka pesa ambazo zilikuwa zimelipwa mapema kwa wasafirishaji wa bidhaa za magendo upande wa Misri wa mpaka, lakini hazikufika.



# OMAR MARMOUSH, "MRITHI WA SALAH", ANAYEKARIBIA KUTUA MANCHESTER

**MANCHESTER City wamefikia "makubaliano ya mazungumzo" na klabu ya Ujerumani Eintracht Frankfurt kumsajili mshambuliaji nyota Omar Marmoush katika kipindi hiki cha majira ya baridi kali, vyanzo kadhaa viliiambia BBC.**

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Misri mwenye umri wa miaka 25 amefunga mabao 20 katika mechi 26 katika mashindano yote akiwa na klabu hiyo ya Ujerumani tangu kuanza kwa msimu wa sasa wa soka.

"Makubaliano ya mazungumzo yameafikiwa kati ya klabu hizo mbili lakini mchakato wa uhamisho bado haujakamilika," duru hizo ziliiambia BBC.

Kutokana na mchezo wake mzuri , Marmoush alikua gumzo la kipindi cha uhamishaji wa msimu wa baridi ulioanza mwanzoni mwa Januari, huku kukiwa na juhudi za vilabu vya Ulaya kumpata.

Uhamisho wa Marmoush kwenda City, ambaye alijiunga na Frankfurt kwa uhamisho wa bila malipo, unakadiriwa kuwa karibu euro milioni 67, kulingana na gazeti la Uingereza la Daily Mail.

Wamisri wanatumai kuzaliwa kwa "Farao" mpya baada ya nyota wa Liverpool, Mohamed Salah

**Safari iliyokaribia kuisha mapema**

Marmoush alizaliwa Cairo mnamo Februari 1999, na alianza maisha yake ya soka katika klabu yake ya Akademi ya Wadi Degla Club na kuendelea na timu hiyo hadi 2017.

"Kipaji chake kiliibuka mapema na akaanza kupanda ngazi hadi timu ya vijana wemye umri mkubwa kwa sababu ya talanta yake," alisema Ali Abu Greisha, meneja wa sekta ya vijana wa Wadi Degla wakati huo.

Mfaransa Patrice Carteron, kocha wa Wadi Degla wakati huo, aliona talanta ya Marmoush na kumpandisha kwenye kikosi cha kwanza mnamo 2016 alipokuwa na umri wa miaka 17.

Mkuu wa Klabu ya Wadi Degla, Hazem Khairat, aliambia BBC kwamba Marmoush amethibitisha ustadi wake tangu mechi yake ya kwanza baada ya kuitwa kwenye kikosi cha kwanza msimu wa 2015/2016, baada ya kuchangia pasi ya uhakika katika ushindi wa 3-2 wa timu yake. Al-Ittihad ya Alexandria katika michuano ya ligi.

Khairat, ambaye amekuwa akifanya kazi katika klabu ya Wadi Degla tangu 2007, alidokeza kwamba bao la kwanza la Marmoush akiwa na Wadi Degla lilikuwa dhidi ya Sharkia msimu wa 2016/2017, ambao ulimalizika kwa mabao mawili bila majibu, na katika msimu huo huo, chini ya uongozi wa kocha Ahmed Hossam Mido wakati huo.

Lakini kazi ya Marmoush ilikaribia kukoma mapema kwa sababu baba yake, ambaye pia ana uraia wa Canada, alitaka mwanawe azingatie zaidi masomo yake.

"Nilishangaa baba yake aliponiambia kwamba Marmoush atakosa mafunzo wakati wa mwaka wa shule kwa sababu ratiba ya mafunzo ilikinzana na siku yake ya shule," Abu Greisha, gwiji wa zamani wa Ismaily alisema. "Omar alipinga uamuzi huu, hivyo niliamua kwa makubaliano na baba yake na uongozi wa klabu kumpanga kocha wa kumfundisha peke yake ili tusipoteze kipaji hiki mapema.

Akiwa na umri wa miaka 18, Marmoush ambaye ana uraia wa Canada, alihamia Ujerumani, ambapo awali aliichezea timu ya akiba ya Wolfsburg, ambayo aliendelea nayo hadi alipopanda kwenye kikosi cha kwanza mwanzoni mwa 2021, mwaka ambao alijiunga na timu ya taifa ya Misri kwa mara ya kwanza.

Mnamo Oktoba 2021, Mreno Carlos Queiroz alimjumuisha katika timu ya taifa ya Misri pamoja na nyota Salah na wachezaji wenzake, baada ya kushinda taji la mchezaji bora chipukizi katika Bundesliga kwa mwezi wa Septemba.

Wakati wake na Wolfsburg, Marmoush alitolewa kwa mkopo kwa St. Pauli, ambayo alicheza katika kitengo cha pili, na kisha Stuttgart.

Kisha akarejea Wolfsburg, ambapo alitumia msimu wa 2022-2023 kabla ya kujiunga na Frankfurt msimu wa joto wa 2023 baada ya mkataba wake na wa zamani kumalizika.

Katika msimu wake wa pili na Frankfurt, Marmoush, ambaye anaweza kucheza katika nafasi kadhaa kwenye safu ya ushambuliaji, alifunga mabao 15 na kusaidia 9 katika mechi 17 za Ligi ya Ujerumani, na pia alifunga bao na kutoa pasi mbili za mabao kwenye Kombe, kabla ya timu yake kutolewa katika hatua ya kumi na sita.

Huko Uropa, alifunga mabao 4 na kutoa asisti 2 kwenye Ligi ya Europa, shindano la pili kwa ukubwa kwa bara katika kiwango cha vilabu, katika mechi 6.Ingawa ni nusu tu ya msimu umepita, Marmoush tayari ameipita idadi yake ya mwaka jana alipofunga mabao 12 na kutoa asisti 6 katika mechi 29.

Kulingana na tovuti ya takwimu ya Opta, Marmoush amekuwa, wakati wa msimu huu, mchezaji wa kwanza katika historia ya Eintracht Frankfurt kufunga mabao 10 katika mechi tisa za kwanza kwenye Ligi ya Ujerumani.

Pia akawa mchezaji wa kwanza kufunga mabao 6 katika raundi tano za kwanza za Bundesliga, rekodi mpya kwa mchezaji kutoka Frankfurt. Alichaguliwa katika timu bora mara 4 katika raundi sita za kwanza.

Marmoush pia amekuwa mchezaji wa kwanza kutoka ligi tano bora za Ulaya kufunga bao kutoka kwa mpira wa adhabu wa moja kwa moja katika mechi tatu mfululizo, tangu Lionel Messi akiwa na Barcelona mnamo 2019.

Akiwa na bao lake la 13 kwenye ligi, Marmoush alikua mchezaji wa tatu kufunga idadi hii ya mabao katika kipindi cha kwanza cha msimu mmoja wa Bundesliga kwa Eintracht Frankfurt tangu 2010.



KUMEKUCHA
MICHEZO
Tovuti: www.kumekucha.co.tz

# Chama atoa ya moyoni Yanga



NA MWANDISHI WETU

**KIUNGO wa Yanga Clutous Chama ameweka wazi kwamba hajawahi kuwa na mgogoro wowote ndani ya klabu yake mpya ya Yanga tangu aliposajiliwa msimu uliopita, badala yake alikuwa majeruhi yaliyomfanya asionekane uwanjani kwa muda mrefu aliokuwa akipatiwa matibabu.**

Kimya cha kiungo huyo raia wa Zambia nd ani ya kikosi cha Yanga kulianza kuzusha mjadala akidaiwa kimya chake kinatokana na kutokamilishiwa madai yake ndani ya klabuy hiyo na kulazimika kuweka mgomo.

Chama ameweka wazo hayo akidai kwamba hawezi kuwaangusha wanayanga kwa vile klabu yao inaheshimu wachezaji na pia ina viongozi waliosoma na wanaojua maana ya mikataba.

Chama hakuonekana katika mechi kadhaa za timu yake hivyo lakini baadaye akionekana akiipigania wakati wa mchezo wao dhidi ya timu ya Al Hilal ya nchini Suda, mchezo uliopigwa nchini Mouritania ambako ndiko was8udau hao waliokoweka maskani yao.

Chama aliingia kipoindi cha pili dakika za mwisho na kujweza kuonyesha uwezo mkubwa baada ya kupeleka shambulizi kali langoni mwa wapinzani kiasi cha mabeki kumzuia kwa mikono, hatua iliyowafurahisha mashabiki na kumtaka kiungo huyo kuendelea kuitumikia timu yao.

Chama alisikia kilio cha mashabiki na kuweka wazi kuwa bado anaipenda klabu hiyo ya wananchi na atatendelea kuitumikia kwa nguvu zake zote.

MWAGITO — SHEDRACK KILASI




# WINGA MPA YANGA KUANZA KUKIPIGA JUMAMOSI

**JONATHAN Ikangalombo winga hatari wa yanga alaiuyesajiliwa kutoka AS Vita kutoka nchini DRC, ataanza kuonekana Jumamosi hii atakapoichezea timu yake, itakayoivaa Gopco FC katika mchezo wa Kombe la ASFA, mchezo utakaopigwa kwenye Uwanja wa KMC mwenge Jijini Dar es salaam.**

Nyota huyo aliyesajiliwa katika kipindi cha usajili wa dirisha dogo anatajwa kuwa anaelezwa ni moto wa kutolea mbali anayeweza kuwakumbusha mashabiki wa timu hiyo makjali ya aliyekuwa mkali wa eneo hilo Tuisila Kisinda.

"Huyu ana kasi zaidi ya Tuisila Kisinda lakini tofauti yeye ana uwezo wa kuingia kati na ana jicho la kupachika mabao kama ilivyokuwa kwa Fiston Mayele" alisema kiongozi mmoja wa Yanga aliuyemnshuhudia nyota huyo makijifua hata hivyo hakutaka jina lake liandikwe gaztini.

Yanga ambayo wiki iliyopita iliwaomba radhi mashabiki wake kutokana na kushindwa kuvuka kihunzi kucheza hatua ya Robo fainali ya michuano ya Klabu Bingwa Afrika sasa imawataka waendelee kuwa karibu na hasa katika mchezo huo ambao utawashuhudia wachezaaji wao wakitoa burudani katika mchezo huo.